

Kiingereza kama Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia Katika Shule za Sekondari Tanzania kinachangia Kuzorota kwa Elimu

Halima Mwinsheikhe na Mwajuma Vuzo

English Summary

This article summarizes two research studies on the medium of instruction in Tanzanian secondary schools. The objective of these studies was to find out how the use of Kiswahili affected student understanding, participation and performance in classrooms. Data was collected by means of interviews, questionnaires, classroom observation and a cartoon comprehension test. Generally, the studies showed that when Kiswahili was used as a medium of instruction, students understood better, explained themselves better and participated much more in class. Performance was likewise improved.

Utangulizi

Lugha mbili zinazohusishwa katika utoaji wa elimu Tanzania ni Kiingereza na Kiswahili. Kwenye shule za awali na msingi, Kiswahili hutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Kingereza hufundishwa kuanzia darasa la tatu kama somo la lazima. Katika shule za sekondari na vyuo Kingereza ndiyo lugha rasmi ya kufundishia na kijifunzia. Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima hadi kidato cha nne.

Kiswahili ni lugha ya taifa, hali kadhalika ni lugha rasmi ya mawasiliano. Kiswahili kinazungumzwa na zaidi ya asilimia tisini na tano (95%) ya watanzania, huzungumzwa aidha kama lugha ya kwanza⁴ au ya pili⁵. Nje ya mipaka ya Tanzania Kiswahili, kimepata umaarufu katika nchi za Africa mashariki na kati, hususan, Kenya ambapo pia ina hadhi ya lugha ya taifa.

Lugha ya kufundishia na kujifunzia baada ya uhuru

Mwaka 1967, Sera ya Elimu ya Kujitegemea ilianzishwa na marehemu Julius Kambarage Nyerere, rais wa kwanza wa Tanzania. Sera hii ilitilia mkazo umuhimu wa Kiswahili kutumika kufundishia katika shule za msingi.

Umuhimu wa kutumia Kiswahili katika shule za sekondari ulizungumziwa kwa mara ya kwanza katika mpango wa maendeleo wa 1969-1974, (URT 1969). Katika kipindi hiki serekali ilihofia kuwa badiliko la lugha ya kufundishia kati ya shule za sekondari na msingi lingewaleta wanafunzi ugumu wa kuelewa masomo mapya kwa lugha mpya ya kujifunzia na kufundishia. Hivo umuhimu wa kutumia Kiswahili katika shule za sekondari ukaonekana kuwa ni muhimu hasa ikizingatiwa mpango wa serikali ulikiwa ni kutumia Kiswahili katika ngazi zote za elimu.

Mpango huu usingefanyika mara moja kwani muda wa maandalizi muhimu ulihitajika. Maandalizi muhimu yalianza kufanyika, kutafsiri kuandaa tamathali za kufundishia. Kwa sasa ukosefu wa istilahi za kitaalam sio tatizo, Mwansoko (1999), Mutasa (2003: 201).

Lugha inayotumika rasmi sasa kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari ni Kingereza, hii ni kwa mujibi wa sera ya Elimu ya mwaka 1995, MoEC (1995). Sera hii kutoka wizara ya elimu na Utamaduni inasema:

Lugha ya kujifunzia na kufundishia katika shule za awali iwe ni Kiswahili na Kingereza kiwe somo la lazima: 35

Lugha ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi iwe ni Kiswahili, na kingereza kiwe somo la lazima: 39

Lugha ya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari iendelee kuwa Kingereza isipokuwa kwa masomo ya lugha. Kiswahili, kiwe ni somo la lazima hadi kidato cha nne: 45 (MoEC 1995, tafsiri yetu)

Hapo hapo Wizara ya Elimu na Utamaduni imetoa sera mpya ya utamaduni, MoEC (1997) ambayo inataja lugha ya kufundishia katika shule za sekondari kuwa ni Kiswahili. Hata hivyo sera hii mpaka sasa haijatekelezwa. Pamoja na kuwa Jones na Rubagumya (1998) walifanya utafiti wa jinsi wa kutekeleza mpango huu na kutoa mapendekezo, mpaka sasa hamna kilichofanyika kutekeleza suala hili. Sababu nyingi hutolewa hasa sababu kubwa ni suala la uchumi kama ilivyo katika ripoti ya maendeleo ya Elimu ya mwaka (1999) ambapo imesemekana kuwa maswala yote yaliyohusu fedha yalisitishwa mpaka hapo serikali itakapopata fedha, suala la lugha likiwemo (MoEC, 1999).

Tafiti nyingi zimeshafanyika katika shule za sekondari kuhusu suala la lugha ya kujifunzia na kufundishia ambazo kwa ujumla zinaonyesha kuwa hali ni mbaya sana. Nyingi ya tafiti hizi zimeonyesha kuwa wanafunzi wanashindwa kujifunza kwa kutumia lugha ya Kiingereza hali kadhalika waalimu nao hushindwa kufundisha kwa kutumia lugha hii. Mjadala huu wa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari Tanzania, sasa una zaidi ya miaka 30.

Madhumuni ya tafiti hizi

Umuhimu wa kufanya utafiti huu ni ili kuweza:

- Kuchunguza jinsi tatizo la lugha ya kufundishia linavyokwaza ufundishaji na ufundishaji wa masomo ya sayansi hususan Biologia
- Kuchunguza ni kwa kiwango gani na wakati gani Kiswahili hutumiwa na waalimu na wanafunzi wakati wa kujifunza masomo.
- Kuanagilia ni jinsi gani kushiriki kwa wanafunzi na matokeo ya wanafunzi ya majaribio

yanavyoathiriwa na utumiaji wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia.

- Kutafuta maoni ya waalimu na wanafunzi kuhusu kutumia Kiswahili rasmi kama lugha ya kufundishia masomo shule za sekondari.
- Kupata mwangaza kuhusu hali halisi kama ilivyo sasa hivi katika hili suala zima la lugha ya kujifunzia na kufundishia.

Maswali yaliyoongoza tafiti hizi

Ni kwa kiasi gani wanafunzi katika vidato vya I, IV na VI wanaelewa na kuweza kujieleza kwa lugha ya Kiingereza?

Ni kwa kiasi gani wanafunzi na waalimu hutumia Kiswahili (kuchanganya na Kiingereza) kunaendelea katika ufundishaji madarasani katika shule za sekondari Tanzania?

Ni hali gani husababisha waalimu na wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi wakati wa masomo?

Ni kwa jinsi gani kushiriki kwa wanafunzi katika vipindi na matokeo yao ya majaribio vinaathiriwa na utumiaji wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia?

Waalimu wa sekondari wana maoni gani kuhusu kukifanya Kiswahili kama lugha rasmi ya kufundishia na kujifunzia katika sekondari na elimu ya juu?

Utaratibu wa tafiti tulizofanya

Tafiti nyingi zimefanyika kuhusu suala hili. Nyingi zimekuwa katika mwelekeo wa kutafuta maoni ya watu kuhusu kutumia au kutotumia Kiswahili kama lugha za kufundishia na kujifunzia.

Katika mwaka 2001 na 2002 Mwinsheikhe na Vuzo wamefanya tafiti mbili katika mwelekeo wa utekelezaji wa sera ya lugha madarasani. Waliohusika katika tafiti hizi ni waalimu wa sekondari, wanafunzi wa sekondari, maafisa elimu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Washiriki wa Utafiti wa Mwinsheikhe (2001)

Katika utafiti aliofanya Mwinsheikhe (2001), alilenga katika masomo ya sayansi hususan Biologia, na iliwahusisha kidato cha kwanza na cha tatu katika shule tatu za Mkoani Dar es Salaam. Idadi ya waalimu waliohusika ni 92 na wanafunzi waliohusika ni 779 ambapo 505 walishiriki kujibu dodoso na 274 walishiriki kwenye jaribio la darasani. Waliohusika kwenye intavyuu ni maafisa elimu 7.

Utaratibu wa Jaribio la darasani

Katika kila kidato mikondo miwili ilichaguliwa, wanafunzi katika mikondo hii walipewa mtihani ya awali ambao ulikuwa katika lugha ya Kingereza. Kila kidato wakiwa na mtihani wao. Kwa kila kidato mkondo mmoja ulifundishwa kwa lugha ya Kiswahili na mkondo mwingine ulifundishwa kwa lugha ya Kingereza. Wakati masomo yakiendelea mtafiti alifanya uchunguzi madarasani kuangalia jinsi ambavyo ufundishaji unaendelea katika lugha hizi tofauti, ili kuweza kubaini tofauti ya jinsi wanafunzi wanavyoshiriki na kuelewa somo la Biologia kwa kutumia lugha hizi mbili tofauti. Jumla ya vipindi vinne kwa lugha ya Kiswahili vilifundishwa, viwili katika kidato cha kwanza na viwili katika kidato cha tatu. Hali kadhalika idadi kama hio ya vipindi ilifundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Mara baada ya hapo

wanafunzi walipewa mtihani: waliofundishwa kwa Kiingereza mtihani ulikuwa kwa Kiingereza na waliofundishwa kwa Kiswahili mtihani ulikuwa kwa Kiswahili.

Matokeo ya hili jaribio la darasani

Katika vidato vyote viwili matokeo ya jaribio la awali ambalo lilikuwa katika lugha ya Kingereza yalikuwa ni hafifu. Katika kidato cha kwanza mtihani wa mwisho umeonyesha tofauti kubwa sana katika matokeo ukilinganisha na yale ya mtihani wa awali kwa darasa lililofundishwa kwa Kiswahili. Wakati darasa lililofundishwa kwa Kiingereza lilionyesha tofauti ndogo. Katika kidato cha tatu kulikuwa na tofauti ndogo kati ya mtihani wa awali na wa mwisho katika madarasa yote mawili, yaliyofundishwa katika Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo tofauti ilikuwa ni ndogo ikilinganisha na ile ya kidato cha kwanza.

Uchunguzi wa madarasani ulionyesha kuwa kiwango cha kushiriki wanafunzi wakati masomo yanaendelea mfano kujibu maswali, kuuliza maswali na kushiriki kwenye majadiliano katika vikundi na darasani kilikuwa ni cha juu zaidi katika madarasa yaliyofundishwa kwa Kiswahili kuliko katika madarasa yaliyofundishwa kwa Kiingereza.

Maelezo ya Matokeo ya Uchunguzi Madarasani

Sababu kuu zilizotolewa na waalimu na wanafunzi zinazosababisha kuchanganya lugha hizi mbili ni, kufafanua kwa kina vipengele muhimu vya mada; kutoa maelezo na maelekezo muhimu yahasuyo mafunzo kwa vitendo, kazi maalum na mazoezi; kuuliza na kujibu maswali na kujadiliana hususani katika katika vikundi. Mfano ya majibu yaliyoandikwa na waalimu katika dodoso ni kama inavyonukuliwa:

Nikisisitiza kutumia Kiingereza wakati wote ninapofundisha huwa ni sawa na kufundisha mawe na siyo wanafunzi. (Mwalimu wa shule CS2, Tafsiri yetu).

Uchunguzi wa madarasani wakati wa masomo ya jaribio kwa lugha ya Kiingereza ulithibitisha kuwa, ingawaje hawakutakiwa kufanya hivyo, wanafunzi walianza kuzungumza Kiswahili mara tu walipoanza shughuli za masomo katika vikundi. Pale walipojaribu kuzungumza Kiingereza, hawakueleweka vizuri. Baadhi ya maelezo ya wanafunzi kwenye dodoso yanaunga mkono matokeo haya. Hali hii ya udhaifu wa wanafunzi katika kushiriki kikamilifu wakati wa masomo yaliyofundishwa katika lugha ya Kiingereza iliwaiki kuripotiwa pia katika chunguzi za Mlama na Mattered (1978), Roy Campbell na Qorro (1987, 1997), Osaki (1995) na Brock Utne (2000).

Matokeo ya Intavyuu

Wote waliohojiwa kwa njia ya intavyuu walisema kuwa wanajua kuwa kiwango kikubwa cha ufundishaji wa sayansi hufanyika kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, kwa jina la utani, Kiswenglish.

Alama za Wanafunzi katika majaribio

Majibu ya waalimu na wanafunzi katika dodoso na uchunguzi wa majaribio ya awali na ya mwisho yaliyotolewa kabla na baada ya masomo ya majaribio yameonyesha kuwa wakati

Kiingereza kilipotumika kama lugha ya kufundushia na kujifunzia wanafunzi wengi walishindwa kujibu maswali yanayohitaji maelezo marefu, hivyo wengi waliruka maswali au walipojaribu kujibu walishindwa kujieleza vizuri. Wakati Kiswahili kilipotumika kama lugha ya kufundishia, maswali ya namna ile ile katika kugha ya Kiswahili yalijibiwa vizuri zaidi na urukaji wa maswali ulikuwa nadra sana. Wanafunzi wote kwa ujumla walimudu maswali ya aina ya kuchagua jibu, au kutoa majibu mafupi sana. Kwa ujumla sababu kubwa ya kutoshiriki kikamilifu kwa wanafunzi katika masomo ya sayansi na kupata alama duni katika mitihani kama ilivyoripitiwa na asili mia 65 ya waalimu, ni tatizo la kutoimudu vyema lugha ya Kiingereza.

Utaratibu wa Utafiti wa Vuzo (2002)

Mahojiano ya Intavyuu yalifanywa na waalimu na maafisa elimu kuhusu suala zima la lugha ya kufundishia na kujifunzia. Wanafunzi walipewa Kibonzo (Tazama ukurasa wa 10). Walijieleza kwanza kwa Kiingereza ambayo ndio lugha rasmi ya kujifunzia na kufundishia, kisha wanafunzi hao wakapewa kibonzo hiki baada ya wiki mbili kukielezea kwa Kiswahili. Huu utafiti ni marudio ya jaribio ambalo lilifanywa na Desai, Z (2001), Afrika Kusini.

Walioshiriki katika utafiti

Katika utafiti huu walioshiriki ni waalim na wanafunzi katika shule za sekondari za serikali pamoja na maafisa elimu. Jumla ya walioshiriki kama sampuli ni watu 60. Wanafunzi 40 waliochnaguliwa kutoka kidato cha I, IV na VI, waalimu 15 na maafisa elimu 5. Vidato hivi vilichaguliwa kwa sababu maalum. Kidato cha kwanza ndio mwanzo wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia na kidato cha IV na VI ni madarasa ya mitihani ya kitaifa.

Matokeo ya Utafiti

Katika kila kidato cha I, IV na cha VI nilichagua hadithi moja nzuri na moja mbaya katika lugha ya Kiingereza pamoja na hadithi ya Kiswahili ya mwanafunzi mhusika. Kama kielelezo hapa nimetoa mfano mmoja katika kila kidato.

Mfano 1: Kidato cha I

Kingereza

One day is not mather is going to market. Balind of thit man student. I am father is going to charch and children too. the market are the Box, Beg, fotball, is money. father is big than children. one day father is going to football. cry when to shoool.

Tafsiri yangu

Siku moja sio mama anakwenda kwa sokoni. Nyuma ya yule mtu mwanafunzi. Mimi ni baba nakwenda kwa kanisa na watoto pia. soko ni boksi, begi, futiboli, ni pesa. Baba ni mkubwa kuliko watoto. Siku moja baba anakwenda futiboli. Nalia niendapo kwa shule.

Kiswahili

Siku moja mzee mmoja alikwenda uwanja wa ndege akiwa na mizigo yake. *Akatokea* kijana mmoja akamuambia yule mzee kuwa angaria hire ndege. Kumbe alikuwa ni mwizi akachukua mizigo ya yule mzee. Akakimbia *vichakani* akafungua ule mzigo wa yule mzee akakuta nyoka kwenye ule mzigo. Yule mzee akaanza kutafuta mzigo wake. Akatokea kijana mmoja akamwambia panda gari langu nikupereke kwa yule kijana aliye kuchukulia mzigo wako. Akaenda mpaka kwa yule kijana akamkuta anafungua mzigo wake akamuonyesha ule mzigo wake yule mzee akakuta ameshafungua. Hakamuhuliza kwa nini humefungua mzigo wangu akamwambia hebu angaria ulicho kiweka kwenye mzigo wako. Akamwambia kwa nini ulihiba mzigo wangu. Akamwambia yule kijana kama hulikuwa hunalitaka sihunge sema nikupe sio kuhiba je hunge kuta mbwa hungesemaje. Akampereka polisi kufungwa.

Mfano wa 2 : Kidato cha IV

Kingereza

One day they was a one man at the Air port whose name was Mr. ALI SAKU. MR Ali SAKU WAS there in order to wait transport from there to the certain place where he want to go/ travel. For a short time the thief was appear and then he can take Ali's bag and run away with it. After run away up to away from MR ALI, thieves was open's the bags. So as when they already open's, the snake was get outside the bag and then it can affect him. So as let me saying that (thief) to get things without parmision is not good for us. When you want something try to communicate with your fellow in order to be helped with him/ her.

Tafsiri yangu

Siku mmoja kulikuwa na mwanaume mmoja kwenye sehemu ya hewa aliyeitwa Bwana ALI SAKU. Bwana Ali SAKU ALIKUWA hapo ili kusibiri usafiri kutoka hapo kwenda sehemu moja aliyotaka kwenda / kusafiri. Kwa mda mfupi yule mwizi akatokea na akachukua begi la Ali na kukimbia nalo. Baada ya kukimbia nalo mpaka mbali na BWANA ALI, wezi wezi wakafungua mabegi. Ili baada ya kufungua, nyoka akatoka nje ya begi na kumdhuru yeye. Ikaniacha nasema kuwa mwizi kuchukua vitu bila ruhusa sio vizuri kwetu. Ukitaka kitu jaribu kuwasiliana mwenzako ili akusaidie na yeye.

Kiswahili

Siku moja alitokea msafiri mmoja katika uwanja wa ndege, ambaye alikuwa akisubiri usafiri kuelekea alikotaka kwenda. Mtu huyo alijulikana kwa jina mzee ALLY SAKU.

Baada ya muda mfupi akiwa pale uwanja wa ndege, walitokea watu wawili ambao ni mtoto na mzee. Watu wale *walitabirika* kuwa ni wezi. Hapo yule mtoto alikwenda moja kwa moja kwa mzee Saku na kumsalimia huku yule mzee *alifanikiwa* kuiba sanduku la mzee Saku. Baada ya kuiba lile sanduku wote walikimbia. Polisi *alijitahidi* kupiga filimbi lakini hawakufanikiwa kuwakamata. Walipovuka barabara, mbali kidogo na eneo la uwanja wa ndege, ndipo walianza kufungua sanduku ili kugawana vitu vilivyokuwemo ndani. *Ghafla* walivyofungua, likatokea joka na *kumdhuru* yule mzee.

Kwa mujibu wa hii habari, tunaelimishwa kwamba tusiwe na tabia ya wizi katika maisha yetu yote. Kwani wizi sio jambo jema, bali mtu huweza kupoteza maisha yake shauri ya wizi.

Kwa hiyo basi, sote yatupasa kufanya kazi kwa bidii ili tuendeleze maisha yetu na siyo *kujishughulisha* na wizi. Kweli wizi ni hatari katika maisha yetu.


Hadithi hii inaonya watu wezi kuacha tabia hii, kwani huweza kusababisha *madhara* makubwa kwao. Kama tunavyoona wale wezi walioiba kapu na kukuta nyoka ambaye angeweza kuwazuru.

Mfano wa 3: Kidato cha VI

Kingereza

In this story there is a person come from another country and arrive at the airport. When he wait for his friends or his relatives two peoples comes and one start to talk with him while another steal or take his bags and thus start to run. The man and police man whirsteling thief. The two people run and take the car out of the airport building. They drive the car for a long distance and stop the car; they opens the bags and see the big snake.

26 A surprise



Tafsiri yangu

Katika hadithi hii kuna mtu kuja kutoka nchi nyingine na fika uwanja wa ndege. Akisubiri marafiki zake au ndugu zake watu wawili waja na mmoja anza kuongea naye wakati mwingine iba au chukua mabegi yake na alafu anza kukimbia. Mwanaume na polisi wakapiga mluzi mwizi mwizi. Hao watu wawili kimbia na chukua gari nje ya jengo la uwanja wa ndege. Wanaendesha gari kwa mwendo mrefu na kulisimamisha; wakafungua hayo mabegi na ona yule nyoka mkubwa.

Kiswahili

Kuna mtu ambaye *amewasili* kwenye uwanja wa ndege akisubiri ndugu zake kuja kumpokea. Wakati mtu huyo amesimama akingojea, mara kunaonekana wezi wawili wakipanga *mikakati* ya jinsi ya kumwibia huyu msafiri kwa hiyo hawa wezi wanapanga mkakati na yule mdogo anajifanya anamuuliza yule msafiri, wakati akiongea naye, yule mwizi mkubwa anachukua ile mizigo na kuanza kukimbia nayo, kwa hiyo wote wawili wanatimua mbio.

Mlinzi wa pale uwanjani anapuliza filimbi kuashiria ya kwamba kuna wezi wameiba mzigo wa mtu na kukimbia nao, kwa hiyo wale wezi *wamefanikiwa kutoweka* na lile boksi ambalo ni mzigo wa yule msafiri. Kwa kutumia teksi ya kwao na hivyo wakwenda na ile taksi mpaka sehemu iliyojificha na kupaki teksi yao na kutoa nje lile boksi ili waangalie kilichomo kwenye boksi lile. Wanafungua boksi lile *wakitarajia* watakuta mali yenye thamani na baadala yake wanakuta kule kwenye boksi kuna nyoka mkubwa aina ya chatu na hivyo wale wezi wanabaki *wakitahamaki* kuona nyoka mkubwa namna ile kwenye boksi lile

Maelezo ya Matokeo ya Zoezi hili la utafiti

Insha za wanafunzi zinaonyesha wazi tofauti katika kujieleza katika lugha hizi mbili; Kiswahili na Kiingereza. Kwa ujumla insha za wanafunzi kwa Kiingereza ni hafifu. Katika vidato vyote wanafunzi wamejieleza vema zaidi kwa Kiswahili ukilinganisha na kwa Kiingereza. Insha za wanafunzi katika lugha ya Kiingereza hazieleweki wakati insha za Kiswahili zinaeleza wazi mtiririko wa kibonzo. Insha za Kiingereza kwa kiasi kikubwa hazikufanikiwa kukieleza kibonzo ipaswavyo, hasa Kidato cha Kwanza ambao wana hali mbaya zaidi katika Kiingereza, (Tazama mfano wa kwanza). Insha za Kiingereza zina makosa mengi ya msamiati, sarufi maumbo na kuwakifisha na matumizi ya nyakati mbalimbali katika vidato vyote. Zinaonyesha wazi jinsi wanafunzi wanavyohangaika kujieleza. Insha za wanafunzi kwa Kiswahili ni ndefu zaidi na zinadhihirisha wazi utajiri wa msamiati walionao wanafunzi na hazina makosa madogo madogo kama za Kiingereza. Misamiati hii haipo kwenye insha za Kiingereza za wanafunzi. (Tazama misamiati imetiliwa mkazo katika mifano niliyotoa). Kuna tofauti ndogo sana kwenye insha za Kiingereza katika Kidato cha IV na cha VI. Hamna tofauti kubwa katika vidato vyote cha Kwanza, Nne na cha Sita katika insha za Kiswahili. Matokeo haya ya Tanzania yalifanana sana na matokeo ya Afrika Kusini japokuwa wanafunzi wa walioshiriki Afrika Kusini katika utafiti sawa na huu ni wa shule za msingi. Inaonekana kuwa wanafunzi wanajieleza vema kwa Kiswahili.

Maelezo ya Matokeo ya intavyuu

Jumla ya waalimu asilimia 60 waliafiki kuwa wanafunzi wana tatizo katika utumiaji wa Kiingereza. Hili tatizo ni kubwa zaidi kidato cha Kwanza ambacho ni cha Kwanza kutumia Kiingereza kama lugha ya kujifunzia na kufundishia. Wanafunzi huwa na kazi kubwa kwani hujifunza misamiati mipya pamoja na kujifunza masomo mapya kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo yake wengi wa wanafunzi hawa hushindwa kumudu masomo. Wakati wanafunzi wengi wanashindwa kufuatilia masomo hawapati msaada wa aina yeyote kutoka kwa waalimu kuboresha uelewaji wa masomo. Suala hili lilisadikiwa na waalimu asilimia 73.

Waalimu asilimia 60 walikubali kuwa waalimu kama wanafunzi pia wana tatizo la lugha ya Kiingereza. Tatizo hili walisisitiza kuwa lipo zaidi kwa waalimu wa masomo ya sayansi

kwani semina za lugha ya Kiingereza huwa haziwalengi. Hali hii ya waalimu sasa inazidi kuzorota.

Sera ya lugha haitekelezwi ipaswavyo. Madarasani waalimu wanafundisha kwa kuchanganya Kiswahili pamoja na Kiingereza, na wanafunzi vile vile wanajifunza kwa kuchanganya lugha hizi mbili. Klaus (2001) anasisitiza kuwa wanafunzi hujifunza vema zaidi iwapo wanaelewa mwalimu anasema nini (Tafsiri yetu). Hivyo, kuchanganya Kiswahili na Kiingereza ni mbinu inayowasaidia wanafunzi kuelewa. Waalimu asilimia 80 walikubali kutumia mbinu hii.

Utafiti ulidhihirisha kuwa japo waalimu na wanafunzi hawamudu vyema lugha ya Kiingereza wengi wanasita kuafiki kuwa Kiswahili kitumike kama lugha rasmi ya kufundishia. Walisisitiza kuwa Kiswahili ni lugha ya sayansi na teknolojia na kuwa Kiswahili hakijawa tayari kuweza kufundishia, suala ambalo tumekanusha kwani vitabu ni vingi na kamusi nyingi zipo tayari kwa taaluma mbalimbali, hivo suala la istilahi sio tatizo (Mwansoko 1999).

Vilevile kuna baadhi ya maafisa wa wizara ya elimu walioshiriki katika utafiti huu ambao wanasita kusisitiza umuhimu wa kutekeleza sera ya Utamaduni ambayo inasema Kiswahili kitumike kama lugha rasmi ya kufundisha shule za sekondari. Watu hawa walitoa sababu zifuatazo zikiwemo sababu za kiuchumi, mitizamo ya watu katika jamii kuhusu Kiswahili pia ni potofu. Hakuna lugha isiyofaa kufundishia, Kiswahili kinafaa kufundishia, hata hivyo waalimu tayari wanafundishia kwa Kiswahili kwa asilimia kubwa madarasani. Hivo ujuzi wa kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia upo wa kutosha. Kuhusu suala la gharama za kutumia Kiswahili ingefaa kama anavyosisitiza Brock-Utne (2000), kuwa kabla hatujatilia maanani suala la uchumi ni vema kuangalia ukubwa wa gharama tunayopata kwa kuendelea kutumia lugha ya kujifunzia na kufundishia ambayo ni kikwazo kikubwa kwa mamilioni ya wanafunzi.

Hitimisho

Tafiti hizi zimeonyesha kuwa wanafunzi na baadhi ya waalimu hawamudu vizuri lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha rasmi ya kujifunzia na kufundishia. Hivo lugha imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufundisha na kujifunza katika shule za sekondari. Imeonekana kuwa wanafunzi na waalimu wanachanganya Kiswahili na Kiingereza madarasani. Kiwango ni kikubwa zaidi vidato vya mwanzo. Utafiti umeonyesha kuwa wanafunzi hawawezi kujieleza vizuri kwa Kiingereza kwa jinsi ambavyo wanaweza kujieleza kwa Kiswahili.

Utafiti umeonyesha kuwa baadhi ya waalimu bado wanashikilia mawazo potofu kuhusu Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Utafiti pia umeonyesha kuwa kuna baadhi ya maafisa elimu wanasita kutekeleza sera ya utamaduni ambayo inasisitiza utumiaji wa Kiswahili kama lugha ya kujifunzia na kufundishia shule za sekondari. Walitoa sababu mbali mbali kutetea mitizamo yao.

Mapendekeko

Kuna umuhimu wa kusisitiza Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia.

Ili utekelezaji wa sera ya Utamaduni uweze kufanikishwa, tutahijatika kufanya yafuatayo:

- Kuna haja ya kubadili mawazo potofu ya watu kuhusu lugha hizi mbili.
- Kuna umuhimu wa kutumia vyombo vya habari kuelimisha watu kuhusu lugha ya kufundishia na vile vile kusaidia kusambambaza misamiati mipya ya Kiswahili kwa jamii.
- Kiswahili kitapoanza kutumika iende sambamba na utaratibu wa kutunga mitihani ya taifa kwa lugha ya Kiswahili

Vilevile, Kiingereza kifundishwe kama lugha ya kigeni, ukizingatia umuhimu wa lugha hii katika mawasiliano ya kimataifa katika karne hii ya utandawazi.

Marejeo

- Brock-Utne, Birgit (2000). *Whose Education for All? The Recolonization of the African Mind*. New York: Falmer Press.
- Desai, Zubeida (2001). Multilingualism in South Africa with Particular Reference to the Role of African Languages in Education. *International Review of Education*, 47.1: 323–339.
- Jones, K. and Rubagumya, C. (1998). *Language for Learning and Teaching in Tanzania*. Dar es Salaam: Ministry of Education and Culture.
- Klaus, D. (2001). The use of indigenous languages in early basic education in Papua New Guinea: A model for elsewhere? Paper presented at the Annual Conference of the Comparative and International Education and Society, Washington DC, 17 March 2001.
- Mlama, P. and Matteredu, (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Katika Elimu ya Juu*. (The need to use Kiswahili as a medium of instruction in higher education). Dar es Salaam: Bajita.
- Mutasa, V. (2003). The Issue of Language of Instruction in Tanzania. In: *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E & D Limited, pp. 197–204.
- MoEC (Ministry of Education), (1995). *Education and Training Policy*. Dar es Salaam: Ministry of Education.
- MoEC (Ministry of Education and Culture), (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam: Ministry of Education.
- MoEC (Ministry of Education and Culture), (1999). *Taarifa ya Mwaka*. 1998/1999. Dar es Salaam: Ministry of Education.
- Mwansoko, H.J.M. (1999). Ukweli Kuhusu Hali ya Tatizo la Istilahi za Kufundishia Elimu ya Sekondari na ya Juu. In Tumbo-Masabo, Z. N. and Chiduo, E. K. F. (eds.). *Kiswahili katika Elimu*. Dar es Salaam: TUKI, pp. 139–148.
- Mwansheikhe, Halima M. (2001). Science and the Language Barrier: Using Kiswahili as a Medium of Instruction in Tanzania Secondary Schools as a Strategy of Improving Student Participation and Performance in Science. M. Phil thesis in Comparative and International Education, University of Oslo: Institute for Educational Research.
- Osaki, Kalafunja M., 2000. Quality of Education in Tanzania: A Focus on Curriculum Standards and Accountability in Schools. Paper presented at the Heads of Secondary Schools Annual Conference, Arusha, 9–13 October 2000.

- Roy-Campbell, Makini, Z. and Qorro, M. (1987). *A Survey of the Reading Competence in English of Secondary School Students in Tanzania*. University of Dar es Salaam: Department of Foreign Languages and Linguistics.
- Roy-Campbell, Makini, Z. and Qorro, M. (1997). *Language Crisis in Tanzania: The Myth of English versus Education*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- URT (United Republic of Tanzania). (1969). *Second Five-year Plan for Economic and Social Development*, 1 July – 30 June 1974. Dar es Salaam: Government Printers.
- Vuzo, M.S. (2002). Pedagogical Implications of using English as a Language of Instruction in Tanzania Secondary Schools. M. Phil. thesis in Comparative and International Education, University of Oslo: Institute for Educational Research.

Notes

- 1 Lugha hii hapa ina maana sawa na lugha mama hasa kwa watu wengi wanaozaliwa mijini na katika familia nyingi ambapo watu wanaona kutoka makabila tofauti. Idadi ya wanaokizingumza Kiswahili kama lugha mama inaongezeka kwa kasi.
2. Hapa tunamaana kuwa watu hawa hukizingumza Kiswahili baada ya lugha zao za Kitamaduni. Inasadikika kuwa Tanzania ina lugha za kitamaduni takriban 120.